SALAMU ZA MHE. ENG. EVARIST NDIKILO, MKUU WA MKOA WA PWANI KWENYE ZIARA YA MHE. RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA UKAGUZI WA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA (STANDARD GAUGE RAILWAY) TAREHE 28 JUNI, 2020

Mhe. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mhe. Isaac Kamwelwe, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

Mhe. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI,

Mhe. Ramadhani Maneno, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani,

Mhe. Assumpter Mshama, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha,

Dkt Leonard Chamriho, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Uchukuzi),

Dr Delphine D. Magere, Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani,

Ndugu Masanja Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania,

Mhe. Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini,

Wah. Madiwani,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Mhe. Rais;

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana hapa leo.

Pili, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Pwani kukukaribisha wewe na msafara wako hapa Mkoani Pwani. Wananchi wa Mkoa wa Pwani wana imani kubwa na wewe kutokana na kazi kubwa uliyoifanya na unayoendelea kuifanya katika kuwaletea watanzania maendeleo.

Mhe. Rais,

Mradi huu wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (*Standard Gauge Railway – SGR*) ni Mradi wa Kielelezo katika Taifa letu na sisi wananchi wa Mkoa wa Pwani tumefaidika na tutaendelea kufaidika sana kutokana na uwepo wa Mradi huu.

Katika hatua za ujenzi kwa mfano, wananchi wa Mkoa wa Pwani wamefaidika katika maeneo yafuatayo: -

(i) Mradi umetoa ajira nyingi za moja kwa moja (*direct employment*) na zisizo za moja kwa moja (*indirect employment*). Wasimamizi wa mradi huu wametueleza katika ajira karibu 7,000 za moja kwa moja, Mkoa wa Pwani uechangia wafanyakazi 295. Aidha, kwenye ajira 35,000 zisizo za moja kwa moja, Mkoa wa Pwani pia umefaidika sana na ajira hizo.

(ii) Makampuni mbalimbali kwenye Mkoa wetu ni sehemu ya Makampuni karibu 500 yaliyoshiriki kwenye mnyororo wa thamani,

ikiwemo uuzaji wa vifaa vya ujenzi kama nondo na marumaru na utoaji wa huduma mbalimbali. Kwa mfano, Kampuni ya AKO Group wanatoa huduma ya chakula, Art Hotel - huduma ya malazi, Coastal Travel – huduma ya usafiri na Kampuni za Lake Steel na Rodhia wanauza nondo.

(iii) Mradi wa SGR umebadilisha hali ya iliyokuwa Miji midogo na kuwa Miji ya kibiashara (*Central business districts – CBDs*); mfano Soga, Kongowe na Mlandizi. Aidha, Kijiji cha Kwala; kutokana na uwepo wa Bandari kavu na Kituo kikubwa cha SGR, kutalifanya eneo lile kuwa Eneo Maalum la Uwekezaji, yaani *Special Economic Zone – SEZ* litakalovutia ujenzi wa viwanda na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

(iv) Serikali kupitia Mradi imejenga Kituo cha kuhifadhia mboga mboga eneo la Ruvu Stesheni (*Freight station*). Uwepo wa kituo hiki utaamsha ari ya kilimo cha mboga mboga katika bonde la Mto Ruvu na kulifanya kuwa kitovu cha biashara hiyo, yaani *Horticultural Zone.*

(v) Halmashauri zetu pia zimefaidika kwa ushuru na uuzaji wa malighafi za ujenzi kama kokoto, vifusi na mchanga. Katika kipindi hiki cha ujenzi Halmashauri ya Chalinze imepata shilingi **3,310,000,000** kutokana na ushuru wa kokoto. Halmashauri Kibaha inatarajia kupata jumla ya shilingi **3,425,372,909.86** ambapo shilingi **3,245,725,183** ni ushuru wa malighafi za ujenzi na shilingi **179,647,726.86** ni ushuru wa huduma (*service levy*).

Fedha hizi hazijalipwa kwenye Halmashauri husika. Halmashauri ya Kisarawe kwa upande wake ilitarajiwa kukusanya shilingi **6,310,710,000** kama ushuru, ambapo shilingi **749,410,000** zimelipwa a wanaendelea kudai shilingi **5,561,300,000** kutoka kwa mkandarasi.

(vi) Manufaa makubwa zaidi yatapatikana baada ya kukamilika kwa mradi huu kwa kuwa utarahisisha sana usafiri wa abiria na mizigo kwenda Dar es Salaam na Mikoa ya bara inayopitiwa na mradi huu.

Mhe. Rais;

Pamoja na manufaa yaliyopatikana na yatakayoendelea kupatikana baada ya kukamilika kwa mradi huu, zipo changamoto zinazotakiwa kufanyiwa kazi ili kuondoa malalamiko miongoni mwa wananchi wanaopitiwa na mradi huu. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Malipo ya ushuru wa malighafi za ujenzi na ushuru wa huduma kwa Halmashauri za Kibaha na Kisarawe unaofikia jumla ya shilingi **8,986,672,909.86** (Kibaha shilingi **3,425,372,909.86** na Kisarawe shilingi **5,561,300,000**). Ushuru huu ungelipwa ungeimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika kufuatilia suala hili tumeelezwa kwamba lipo kwenye hatua mbalimbali za majadiliano.

(ii) Malipo ya fidia kwa ajili ya Taasisi na Wananchi ambao maeneo yao yameguswa kutokana kupisha ujenzi (upanuzi wa njia ya reli

(extra widening), kuchimba mashimo ya udongo na mengine kumwaga vifusi *(dump sites)*. Madai ya fidia yapo kama ifuatavyo:-

a) Zahanati ya Kijiji cha Minazi Mikinda iliyopitiwa na njia ya umeme inatakiwa kuhamishwa. Uthamini umefanyika na shilingi **167,471,400** zinatakiwa kulipwa kufidia jengo la Zahanati na shilingi **11,798,244** kwa ajili ya choo na kichomeo cha taka *(incinerator).*

b) Jumla ya wananchi 441 wa Kijiji cha Kwala wametambuliwa na kuthaminiwa mali zao, ambapo wanadai jumla ya shilingi **428, 941,600.**

c) Jumla ya Wananchi 273 wa Vijiji vya Mpiji, Mnemela Kibaoni, Soga, Makotopora, Ngeta, Kikongo, Mperamumbi, Minazi Mikinda, Magindu na Mizuguni wanadai fidia ya shilingi **1,785,091,200** kutokana na maeneo yao kumegwa kuongeza upana wa njia ya reli *(extra widening)*

Katika eneo hili la fidia, tumeendelea kufanya mawasiliano na Shirika la Reli Nchini kuhusiana na fidia hizi na maelezo ni kwamba wapo kwenye majadiliano na Wizara mama ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili malipo husika yaweze kufanyika. Hata hivyo, napenda kutumia fursa hii kuishukuru sana Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Shirika la Reli Nchini kwa kuihamisha na kuijenga upya Shule ya Msingi Mahundi kwa thamani ya shilingi 885,000,000. Shule hii ni ya kisasa na ina huduma zote, ikijumuisha

vyumba 16 vya Madarasa, ofisi mbili (2) za Walimu, nyumba tisa (9) za Walimu, vyoo matundu 28, Jengo la Shule ya Awali, Viwanja vya kisasa vya michezo yote na uwekaji wa huduma za maji na umeme.

(iii) Mwisho, katika eneo la changamoto ni malalamiko ya wananchi wa Vijiji cha Kwala na Msua Stesheni kutokana na tuta la reli kuwatenga wananchi na huduma muhimu kama shule, mnada, eneo la makaburi, viwanja vya michezo na kuwalazimisha wananchi kutembea kilometa 6 hadi 7 kufuata huduma hizo. Aidha, huduma za maji na umeme zimekatwa katika maeneo hayo. Tumewasiliana na wahusika na maelezo ni kwamba mkandarasi ameelekezwa kujenga vivuko na kurejesha huduma za maji na umeme.

Mhe. Rais;

Pamoja na changamoto nilizozitaja, Serikali hii ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wako imefanya mambo makubwa sana katika sekta zote na yanaleta matumaini kwa wananchi kushuhudia mabadiliko makubwa sana katika nyanja zote za maendeleo hususani ukuaji wa uchumi, uimarishaji wa miundombinu na huduma za jamii.

Mhe. Rais,

Baada ya kusema hayo nikushukuru wewe na msafara wako kwa kututembelea Mkoa wa Pwani. Tunakutakia kila la heri katika majukumu makubwa yaliyopo mbele yako, hasa Uchaguzi Mkuu ujao na majukumu mengine ya kuwahudumia Watanzania. Tunakuombea kwa Mungu

uendelee kuwa na afya njema ili uweze kutekeleza majukumu haya muhimu.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

ENG. EVARIST NDIKILO
MKUU WA MKOA WA PWANI